# Management Sciences for Health/TFDA Strategies for Enhancing Access to Medicines (SEAM) 2000 - 2004

Mkakati wa Kuboresha Upatikanaji wa Dawa (SEAM) na Tathmini ya Sekta ya Dawa - 2001

# Madhumuni ya Mada Hii

1. Kuelezea maana ya SEAM
2. Kuelezea Matokeo ya Tathmini ya Sekta ya dawa ya Mwaka 2001
3. Kuelezea chimbuko la kubuniwa kwa mpango wa kuboresha Maduka ya dawa Baridi

# Maana ya SEAM

- SEAM – Strategy for Enhancing Access to Medicines – Mkakati wa Uboreshaji wa Upatikanaji wa Dawa

# Malengo ya SEAM/MSH

- Kufanya majaribio ya mikakati ya kuboresha upatikanaji na matumizi bora ya dawa katika nchi mbili au tatu zinazoendelea
- Kutoa uwezo wa kitaalamu wa kusimamia vizuri huduma za dawa

# Mfumo wa utekelezaji wa SEAM/MSH

- Kuendeleza na kuanzisha mipango au mbinu ambazo zinaimarisha uwezekano wa jamii kupata mahitaji muhimu ya afya kwa kutumia zaidi miundo na huduma za binafsi
- Kuimarisha ubora wa huduma za binafsi za dawa ili ziweze kusaidia kutekeleza malengo ya afya ya Taifa

# Uchaguzi wa Nchi

- Tanzania
- Ghana
- Cambodia
- Rajastan (India)
- El Salvador
- Minas Gerais (Brazil)
- Nchi katika rangi nyekundu ndizo zilizochaguliwa

# Tathmini ya Sekta ya Dawa -Tanzania (1)

- Dar es Salaam – Temeke, Kinondoni
- Masasi
- Njombe
- Karagwe
- Kilimanjaro Vijijini
- Tanga Mjini
- Dodoma Mjini

# Masuala Kuhusu Upatikanaji wa Dawa Tanzania ni Yapi?

- Kuwepo kwa dawa (availability)
- Uwezo wa kununua dawa hizo (affordability)
- Umbali (geographical accessibility)
- Ubora (quality)
- Kukubalika na Kuridhika (acceptability/satisfaction

# Umbali (Geographical Access)

| | 1980 Vituo vya umma | 1999 Vituo vya Umma | Maduka Binafsi |
|---|---|---|---|
| Km 1 | 45% | 46% | 61% |
| Km 5 | 72% | 73% | 86% |
| Km 10 | 93% | 86% | 94% |

# Upatikanaji (Availability)

| PHC Level | |
|---|---|
| **Product** | **Avg % time O/S** |
| Amoxycilin 250mg | **30%** |
| Benzylpenicillin | **19%** |
| Chloroquine 300mg | **9%** |
| Condoms each | **12%** |
| Co-trimoxazole 480 | **32%** |
| Depo-Privera vial | **23%** |
| Doxycyline 100mg | **21%** |
| Examination Gloves | **28%** |
| Ferrors Sulphate | **14%** |
| Mebendazole 100mg | **23%** |
| Metromidazole | **23%** |
| Needle 22G + | **31%** |
| ORS | **10%** |
| Oxytetracycline Eye | **13%** |
| Paracetamol 500mg | **31%** |
| Polio Vaccine vial | **17%** |
| | |
| **Average** | **21%** |
| Source: SEAM 2001 | |

# Mutasari wa Matokeo ya Tathmini - Ubora (Quality) 1

- Tathmini imeonyesha kuwa bado kuna matatizo kuhusu ubora wa baadhi ya dawa zilizoko kwenye soko la Tanzania.

# Muhtasari wa Matokeo
# Ubora wa Huduma (2)

- Ubora wa  Huduma
  - Huduma zitolewazo hasa katika maduka mengi ya dawa baridi ni finyu na haziridhishi

# Muhtasari wa Matokeo - Affodability -Uwezo wa kugharamia dawa (3)

- Watanzania wenye kipato kidogo wanalazimika kufanya kazi muda mrefu ili wapate fedha za kuweza kununua dozi moja ya dawa muhimu kutibu  magojwa kama:
  - Malaria
  - Kichomi
  - Minyoo nk.

# Changamoto

- Kuboresha upatikanaji wa dawa kwenye sekta ya umma
- Kuboresha ubora wa dawa na huduma pamoja na kuangalia uwezokano wa kununua dawa hizo hasa katika sehemu za vijijini kwa bei nafuu.

# Mikakati

- Kuboresha huduma ya dawa vijijini kwa kuanzisha maduka maalumu Accredited Drug Dispensing Outlets (ADDO)
- Kuongeza/kuboresha mbinu za kudhibiti dawa zinazoingia kutoka nje na zile za ndani

# Mkakati wa Mpango wa ADDO (1)

- Kuendeleza mpango wa kuhimiza uanzishaji wa maduka ya dawa madogo (ADDO) yatakayosajiliwa na TFDA
- Maduka hayo yatauza dawa zitakazokidhi mahitaji ya msingi, hasa vijijini/miji midogo,
- Dawa zitakuwa na ubora unaokubalika na pia kutoa haduma bora ya kitaalamu katika mikoa yote ya Tanzania

# Mkakati wa Mpango wa ADDO (2)

- TFDA itaweka vigezo (standards) kuhusu:
  - Ubora wa dawa,
  - mafunzo,
  - ukaguzi na usimamizi
  - orodha ya dawa,
  - ushauri wa afya na taarifa zinazohusu dawa na huduma inayotolewa
- Aina za dawa zitakazouzwa zitafanana na zile zilizomo kwenye masanduku ya dawa za zahanati/kituo cha afya
- Sheria na udhibiti:
  - TFDA ikisaidiwa na Mamlaka mbalimbali za mkoa, wilaya hadi kata itadhibiti ufuatiliaji wa sheria na ubora wa huduma

# Mkakati wa Mpango wa ADDO (3)

- **Kuhamasisha kuhusu mradi:**
  - Watendaji wakuu wa mkoa,
  - wilaya,
  - serikali za mitaa,
  - wamiliki/wauzaji wa maduka ya dawa baridi,
  - Vikundi mbalimbali vya jamii nk.
- **Mafunzo ya kina yatatolewa**
  - Kwa wafanyakazi wa maduka hayo
  - Kwa wenye maduka.
- **Kuendeleza ADDO katika mikoa mingine**

# Kudhibiti Ubora wa Dawa (1)

- Kuanzisha/Kuendeleza njia na uwezo wa TFDA wa kuchunguza ubora wa dawa:
  - Zinazotengenezwa nje na ndani ya nchi
  - Kwa haraka na kwa gharama nafuu
  - Kuzuia zile ambazo hazikidhi ubora unaotakiwa kuwepo katika soko la Tanzania

# Kudhibiti Ubora wa Dawa (2)

- Mategemeo:
  - Kuongezeka kwa idadi ya dawa zilizohakikiwa kimaabara
  - Kupunguza idadi ya dawa zisizo na ubora katika soko
  - Tanzania kuwa na mpango mzuri wa udhibiti wa ubora wa dawa na hivyo kuwa kioo na kuweza kuigwa na nchi nyingine

# Mchango wa MSH-RPMPlus

- Kutoa ushauri wa kiufundi na kiutalamu na pia kukodi watalamu kufanya kazi maalumu
- Kushauri mbinu au kutoa nyenzo za kuendeshea na utekelezaji wa mpango wa DLDM
- Kutoa mafunzo mbalimbali
- Kuimarisha mawasiliano na jamii kuhusu matumizi bora ya dawa